

Swahili transcript:

Watanzania pia tuna vazi hili la kitenge, na vazi hili la kitenge linapendwa na watanzania karibu wote. Kama ambavyo mnaniona, nimevaa vazi hili la kitenge, nimeshona, hii ni blauzi, ni blauzi ambayo imeshonwa na hiki ni kitenge nimefunga, pamoja na hiki pia ni kitenge kwa juu, nimefunga kichwa. Kwa hiyo ukifika Tanzania, utawakuta akina mama wengi sana wanapenda kuvaa vazi hili la kitenge. Na vazi hili la kitenge, wanawake wanavaa sehemu mbalimbali, kama kwenye sherehe mbalimbali labda sherehe za harusi, na sherehe nyinginezo. Pia vazi hili watanzania wanawake, hususani wanawake wanavaa pia makanisani au sehemu nyingine za mikusanyiko. Kwa hiyo ni vazi ambalo watanzania wengi hususani wanawake wanapenda sana kuvaa vitenge. Na kama ambavyo nimesema, hiki ni kitenge, kimeshonwa, hii ni blauzi imeshonwa, kwa hiyo na wanaume pia wanavaa vitenge. Wanaume wao wanashona mashati, pia wanashona na suruali. Kwa hiyo wanaume utawakuta wamevaa mashati ya kitenge pamoja na suruali za kitenge. Vilevile wakina mama pia au wanawake wengine wanapenda pia kushona mashati pamoja na suruali za vitenge. Kwa hiyo utakuta wanavaa shati pamoja na suruali ya kitenge, au anashona blauzi kama hii ya kwangu pamoja na sketi, au anashona blauzi kama hii ya kwangu, kitenge kingine anafunga kama ambavyo nimefunga. Hiki ni kitenge nimefunga, nimevaa blauzi halafu pia nimefunga na hiki kitenge kwa chini, na kitenge kingine nimefunga kichwani. Kwa hiyo inategemea na jinsi ambavyo yule mtu anapenda kuvaa. Wako wengine pia ambao wanashona kitenge pamoja na pensi, hasa wakina baba utawakuta wengine wamevaa shati la kitenge pamoja na pensi. Na wako wakina mama wengine ambao wanashona shati pamoja na pensi, kwa sababu vazi hili la kitenge ni vazi ambalo linavaliwa na kila mtu. Yaani haijalishi ni wanaume au ni wanamke, kila mmoja anavaa vazi hili la kitenge kule Tanzania, inategemea na jinsi ambavyo yule mtu anataka vazi lake liwe. Kwa sababu tuna mafundi vyerehani ambao ndio tunakwenda kwao na tunawaambia kwamba kwa mfano mimi nataka nguo yangu ishonwe namna hii, kwa hiyo yule fundi anachukua vipimo, baadae anakushonea ile nguo ambayo wewe umetaka iwe. Kwa mfano ukitaka tu blauzi na kitenge, basi anashona ile

blauzi vizuri pamoja na kitenge. Au ukitaka labda ushone l gauni, pia unaweza ukashona gauni la kitenge, au ukitaka kushona suruali pamoja na shati la kitenge, unaweza pia ukashona suruali pamoja na shati hilo kutokana na jinsi ambavyo wewe mwenyewe unataka nguo yako iwe. Nguo hizi za vitenge pia huvaliwa na watoto wadogo. Pia nao wanashona labda kama ni magauni kama kwa watoto wa kike au suruali na shati kwa watoto wa kiume, inategemea na jinsi ambavyo kila mmoja anapenda mtoto wake avae nguo ya aina gani. Kwa hiyo kwa kifupi vazi hili la kitenge ni vazi zuri na linapendwa na watanzania walio wengi. Na ukifika Tanzania, utakuta wanawake na wanaume na watoto wote wanavaa vazi hili la kitenge.

English translation:

Tanzanians have this kind of dress we call *kitenge*, and most Tanzanians like it and wear it. As you can see, this is *kitenge*, and this is a blouse which has been made by a tailor. This is also *kitenge*. I wrapped it around myself and I wrapped another *kitenge* around my head. If you get a chance to come to Tanzania, you will find that many women wear this kind of dress. This is a style women wear on different occasions, such as for wedding ceremonies, at church and other gathering places. So it is a kind of dress that is preferred by many Tanzanians, particularly women. As I said, this is a blouse made from *kitenge*. Men also wear *kitenge*. Men make shirts and trousers, so you will find men wearing shirts and pants made from *kitenge* cloth. There are some women who prefer wearing shirts and pants made from *kitenge* cloth. Others make blouses like this, and skirts, or they can make a blouse like this, and another makes *kitenge* wrap as I have wrapped. This is a *kitenge* cloth I have wrapped, and this is a blouse, and this also a *kitenge*, which I have wrapped around my head. So it depends on how a person wants to wear it. Some prefer to make shirts to wear with shorts, especially men. Some women also make shirts and shorts, because *kitenge* dress is worn by many Tanzanians. All men and women wear *kitenge*. It depends on what you want your dress to look like, because we have tailors who make different types of dresses. We tell them how we want our clothes to look, then they take measurements and make dresses with sewing machines, according to what we want. For example, if you just want a blouse, he will make it, or if you want a gown, or a

shirt and a trouser, you can choose that. This *kitenge* dress can also be worn by small children. Little girls can wear gowns, and little boys can wear shirts with pants. It depends on what you want your children to wear. In short, *kitenge* is a good style and many people like it. Therefore, if you have a chance to visit Tanzania, you will find men, women, and children wearing *kitenge*.

About CultureTalk: CultureTalk is produced by the Five College Center for the Study of World Languages and housed on the LangMedia Website. The project provides students of language and culture with samples of people talking about their lives in the languages they use everyday. The participants in CultureTalk interviews and discussions are of many different ages and walks of life. They are free to express themselves as they wish. The ideas and opinions presented here are those of the participants. Inclusion in CultureTalk does not represent endorsement of these ideas or opinions by the Five College Center for the Study of World Languages, Five Colleges, Incorporated, or any of its member institutions: Amherst College, Hampshire College, Mount Holyoke College, Smith College and the University of Massachusetts at Amherst.

© 2003-2008 Five College Center for the Study of World Languages and Five Colleges, Incorporated